# ARUSHA

## FURSA LUKUKI

# Endless Opportunities

Toleo la Mtandaoni: 06 Tarehe 28/02/2023



# Kazi Iendelee

UTALII, KILIMO, BIASHARA NA UZALISHAJI

# Kazi Iendelee



**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN AKIWA NA WAZIRI MKUU MHE. KASSIM MAJALIWA, SPIKA WA BUNGE DKT. TULIA ACKSON, KAMISHNA WA MAADILI JAJI MHE. SIVANGILWA MWANGESI, KATIBU MKUU KIONGOZI DKT. MOSES KUSILUKA KATIKA PICHA YA PAMOJA NA NAIBU MAWAZIRI WALIOAPISHWA IKULU CHAMWINO MKOANI DODOMA TAREHE 27 FEBRUARI 2023.**

#Uongozi Makini




# TENGENEZENI BIDHAA ZENYE KULETA USHINDANI KATIKA SOKO

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha ,Bwana Missaile Musa amewataka Wakurugenzi wa Halmshauri za Mkoa wa Arusha kubaini vikundi vinavyojihusisha na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ili viweze kupata mafunzo kutoka Tume ya Ushindani (FCC) kwa lengo la kuongeza tija ikiwemo mnyororo wa thamani kwaajili ya kuleta ushindani wa soko.

Agizo hilo limetolewa hivi karibuni Jijini Arusha na Katibu Tawala Musa wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya uhamasishaji wa masuala ya ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia kwa wazalishaji Kanda ya Kaskazini. Alisema endapo vikundi vinavyopewa mikopo na Halmashauri vikipata mafunzo ya udhibiti wa ushindani wa kibiashara vitawezesha bidhaa zao kuingia katika masoko ya ndani na nje kutokana na ubora, pia ameziтaka Halmshauri zishirikiane na FCC katika kuleta ushindani wa thamani za ubora wa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wanaopata mikopo ya 10% ya Halmshauri".

Kwa upande wake Mkuu wa FCC Kanda ya Kaskazini,Bwana Nonge Juma alisema, mafunzo hayo kwa wafanyabiashara wa Viwanda vidogo, vya kati na vikubwa yanalengo la kuwezesha kuleta tija katika ushindani wa biashara wa bidhaa wanazozalisha ikiwemo kudhibiti bidhaa bandia zisizizosajiliwa na kuleta athari kiuchumi.

Aidha, bwana Nonge alisisitiza kuwa wafanyabiashara hao na wale wenye viwanda kuhakikisha wanazingatia taratibu za kisheria na maadili ya biashara ili kuhakikisha soko linabaki kuwa shindani .

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho la Viwanda Tanzania Mkoa wa Arusha(CTI), Bwana Anup Modha alitoa rai kwa wamiliki wa Viwanda na Wafanyabiashara mbalimbali kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kuleta ushindani katika masoko kwa kuzingatia ushindani wa masoko ya ndani na nje ya nchi.

Tume ya Ushindani imeandaa mafunzo hayo kwa lengo la kuwajengea uwezo wazalishaji wa bidhaa ili waweze kuingia katika soko la ushindani hasa nje ya Nchi na kuweza kukuza biashara zao



# WAZIRI NAPE ARIDHISHWA NA HATUA YA UJENZI WA JENGO LA MAKAO MAKUU YA UMOJA WA POSTA AFRIKA (PAPU).

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,Nape Nnauye amezitaka Taasisi zinazotoa Huduma za maji na umeme kuongeza kasi ya kufungua mifumo hiyo kwaajili ya jengo la Umoja wa Posta Afrika (PAPU) ili liweze kukamilika kwa wakati na kuleta taswira nzuri kwa Jiji la Arusha

Waziri Nape aliyasema hayo Jijini Arusha wakati wa ziara yake ya kutembelea na kujionea hatua za mwisho za umaliziaji wa jengo hilo lenye ghorofa 18 linalojengwa Jijini Arusha eneo la Philips.

Alisema Serikali ya Tanzania imetoa asilimia 40 ya gharama za ujenzi huo kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) huku asilimia 60 imechangiwa na Nchi wanachama wa PAPU.

“Jengo hili litakamilika Aprili mwaka huu 2023 na hapa naagiza watoa huduma za maji na umeme kuharakisha huduma hizo mara moja ili jengo hili liweze kukamilika kwa wakati ili liweze kutumika kwa wakati.”

Aidha, Waziri Nape ameushukuru Uongozi wa Rais Samia Hassan Suluhu kwa kuhakikisha jengo hilo la Makao Mkuu ya PAPU linajengwa Nchini Tanzania na kusisitiza kuwa jengo hilo litakuwa linatoa huduma za posta kidigitali zaidi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa PAPU,Dk,Sifundo Chief Moyo alisema uamuzi wa Umoja huo kuamua kujengwa jengo hilo Nchini Tanzania ni fahari kwa Nchi, sanjari na Wanachama wengine kwani utaongeza chachu ya kusukuma mbele maendeleo ya utoaji huduma za haraka kwa Nchi za Afrika.

Vile vile kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella alisema ujenzi wa jengo hilo utawezesha mkoa kunufaika kiuchumi na kubadilisha taswira ya Mkoa kwani Taasisi nyingi zitapata nafasi ya kuwa na Ofisi zao katika jengo hilo.



# MADIWANI JIJI LA ARUSHA KUTATUA CHANGAMOTO YA UMEME, MAJI NA BARABARA

Madiwani wa Jiji la Arusha wamemuomba Mkuu wa Wilaya ya Arusha Felician Mtahengerwa kuwaita Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (Auwsa) na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kukaa meza moja ili kujadili changamoto za maji,barabara na umeme.

Wametoa ombi hilo hivi karibuni Jijini Arusha katika kikao cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/23 cha Madiwani ,Madiwani hao kutoka kata 25 za Jiji la Arusha walikubaliana kutoa mwezi mmoja ili taasisi hizo zikutane na madiwani hao na kujadili changamoto za wananchi.

Kwa upande wake, Diwani Doita akihoji kwanini Tarura hawatengenezi baadhi barabara mbovu na msimu unaokuja ni msimu wa mvua hivyo hali ni mbaya kwenye baadhi ya barabara za mitaa na kuleta usumbufu kwa watoto wa shule, watu wazima na vyombo vya usafiri.

Diwani Marti alihoji ni kwanini hadi sasa Auwsa hawajafukia mitaro ya mabomba iliyochimbwa ya maji safi na salama Jijini Arusha na kusababisha mitaro hiyo kuwa njia za maji wakati wa mvua kali za masika na kusababisha kero kubwa kwa wananchi.

Naye Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (Auwsa), Masoud Katiba alisema Mamlaka hiyo inaendelea kutoa huduma mbalimbali za maji kwa Wananchi wa Jiji la Arusha na viunga vyake pia kutatua changamoto zao.Aidha Auwsa itaendelea kuboresha huduma zake kwa wateja wake wote kwa kuzingatia sheria na taratibu.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Arusha,James Lobikoki alisema Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji itawasiliana na Mamlaka husika ili waweze kujadili na kutatua changamoto hizo kwa pamoja na kuwaondolea kero Wananchi wa Jiji la Arusha.

Wakati huo huo, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa aliagiza Jiji la Arusha kuhakikisha taa za barabarani zinawaka kuanzia saa moja usiku hadi asubuhi kwani Jiji hilo ni Jiji la Utalii na linapaswa kuendelea kufanya shughuli za biashara nyakati zote pasipo bughudha za kiusalama.

“Arusha ni Jiji la Mikutano na lango la Utalii,hatuwezi kuona mitaa yake inakuwa giza,hii inahatarisha usalama wa raia na wageni wetu,naagiza Jiji fungeni taa mitaa yote.” Alisema Mtahengerwa.



# KITUO CHA KUSHIKILIA WATUHUMIWA NA WAFUNGWA WA MAUWAJI YA KIMBARI CHA KABIDHIWA KWA SERIKALI YA TANZANIA

Kamishina Jenerali wa Magereza Mzee Ramadhani Nyamka amesema kuwepo kwa kituo cha kushikilia watuhumiwa na wafungwa wa mauwaji ya Kimbari kilichokuwa kikisimamiwa na Umoja wa Mataifa kimeleta faida kubwa kwa baadhi ya maafisa wa polisi kuongeza ujuzi katika utendaji wao wa kazi.

Ameyasema hayo hivi karibuni alipokuwa akipokea kituo hicho kwa niaba ya Serikali ya Tanzania kutoka kwa Msajili wa Mahakama ya Masalia ya Kesi ya mauwaji ya Kimbari Abubacarr Tambadou.

Kamishina Jenerali Nyamka, amesema kurudishwa kwa kituo hicho kwa Serikali ya Tanzania kutasaidia kupunguza msongamano katika magereza ya Tanzania kwani baadhi ya wafungwa watahamishiwa katika kituo hicho na kuwa majengo hayo yana hadhi ya Kimataifa katika kuhifadhi watuhumiwa na wafungwa.

Kamishina Jenerali Nyamka amesema Tanzania ilishasaini mikataba ya Kimataifa ya namna ya kutunza Wafungwa na huduma gani wapate, hivyo mpango wa Serikali ni kuhakikisha Magereza yote Nchini yanafuata makubaliano hayo ili yaweze kufanana na kituo hicho.

Uzoefu uliopatikana kwa Jeshi la Magereza kupitia kituo hicho ukitumika katika Magereza mengine utaongeza ufanisi wa kazi na utaleta maendeleo katika Magereza hayo.

Maafisa waliopata uzoefu huo watatumika kama Walimu kwa wengine ili kupata uelewa zaidi wa shughuli za Magereza.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella amesema kituo hicho kitasaidia kuongeza uwezo kwa Gereza la Kisogo katika kutoa huduma kwa watuhumiwa mbalimbali na wafungwa.

Aidha, amesema Serikali ya Mkoa itaendelea kushirikiana na mfumo wa Magereza kuhakikisha eneo hilo linasimamiwa vizuri.

Kituo cha kushikiria watuhumiwa na wafungwa wa mauwaji ya Kimbari kilianzishwa Mkoani Arusha mwaka 1996 chini ya Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.



# ELIMU YA LISHE IKATOLEWE KATIKA NGAZI ZOTE.

Waratibu wa lishe ngazi ya Mkoa na Halmashauri Mkoani Arusha wametakiwa kwenda kutoa elimu ya lishe katika maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye nyumba za Ibada, mashuleni,minadani na kwenye kamati za lishe za Kata.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella alipokuwa akizungumza na Kamati ya lishe Mkoa wakati wa kikao kazi cha tathimini ya lishe ngazi ya Mkoa.

Mongella amesema kuwa tathimini inayofanyika katika viashiria vya lishe haitoshi kujitathimini na kujihakikishia kuwa elimu ya lishe inayotolewa imewafikia wananchi kwa kiwango kikubwa,bali mikakati madhubuti inatakiwa ijengwe mpaka kwenye ngazi ya Kaya kwa kuhakikisha kila mzazi ananatambua umuhimu wa lishe kwa familia.

Katika kusisitiza hilo amewataka Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kwenda kusimamia agenda ya lishe kwa umakini ikiwemo kuhakikisha vikao katika ngazi zao vinafanyika kwa wakati na Wananchi wanapata uelewa wa kutosha kuhusu faida ya lishe wa Jamii.

“Ndugu zangu suala la lishe tusifanye nalo mchezo, lina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya Nchi,lishe bora ndiyo inayochangia ustawi wa afya ya mwili na akili kwa watu wetu kwani ndipo wanapopatikana wataalamu mbalimbali katika sekta zote.” Alisema Mongella

Akichangia mjadala huo,Katibu Tawala wa Wilaya ya Arumeru James Chembe amesema katika kushughulikia suala la lishe ni vyema wataalamu kama maafisa Kilimo na Mifugo wakashirikishwa kwenye mpango kazi kwani kada zao zina mchango mkubwa katika masuala ya lishe bora.

“Hapo zamani tulikuwa tuna utaratibu kwa kila Kaya kuwa na bustani za mbogamboga na kuwa Mifugo ambayo ilisaidia upatikanaji wa vyakula vya lishe na maziwa,nashauri kurudishwe utaratibu wa kulima bustani katika shule zetu ili wanafunzi waweze kupata chakula bora wakiwa majumbani na shuleni.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Arusha, Sulemani Msumi amesema kuna haja ya kutungwa sheria itakayowabana wazazi ambao watakaidi kuchangia fedha za chakula katika shule ili wanafunzi waweze kupata chakula cha mchana kwani hii itasaidia kupunguza wimbi la watoto wengi kukosa chakula shuleni.




# MKUU WA WILAYA YA LONGIDO AKABIDHIWA MADARASA MAWILI NA OFISI MOJA TOKA WORLD VISION

Mkuu wa Wilaya ya Longido Mhe. Marco Ng'umbi ameshiriki Hafla ya kupokea Madarasa Mawili na Ofisi moja iliyojengwa na Wadau wa Maendeleo Shirika la World Vision Tanzania Kijiji cha Loondolwo, Tarafa ya Ketumbeine.

Katika Hafla hiyo Mratibu wa Shirika la World Vision Clusster ya Ketumbeine kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu Bi. Peruth Daudi amesema Wamefadhili Mradi huo baada ya kuona Watoto wakipata Changamoto ya kutembea umbali mrefu kwenda shuleni na wao kama Shirika wameunga mkono Juhudi za Serikali katika kuwaletea Maendeleo Wananchi wa Wilaya ya Longido kwenye Sekta ya Elimu.

Akimkaribisha Mkuu wa Wilaya kuzungumza na Wananchi wa Kijiji cha loondolwo naye Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Longido Bwa. Boniphace Lugola amewashukuru Wafadhili hao kwa kujenga Madarasa hayo na Ofisi na kuwaomba wapeleke Miradi ya Maendeleo Tarafa zingine za Wilaya ya Longido baada ya Muda wa Miradi hiyo kuelekea kumalizika Mwaka huu 2023 kwenye Tarafa hiyo.

Mhe. Ng'umbi amewapongeza za Shirika la World Vision Tanzania kwa juhudi zao za kuiunga mkono Serikali kwenye Sekta ya Elimu, Afya na Maendeleo ya Jamii hasa Wilaya ya Longido, Tarafa ya Ketumbeine, amewaomba waendelee na Juhudi hizo na Serikali itawapa Ushirikiano wote itakaohuitaji.

Aidha, Mhe. Mkuu wa Wilaya amewaagiza Wazazi kuwapeleka Shuleni Watoto wao na si kuwatumikisha kazi za Nyumbani ili Adhima ya Wafadhili ya kujenga Miundombinu ya Elimu iweze kutimia na si kuyaacha Madarasa hayo kama Maghofu bila kutumika.



# TUNZENI MAZINGIRA YA VYANZO VYA MAJI. (KARATU)

Mkuu wa Wilaya ya Karatu Dadi Kolimba amewataka wananchi wa Karatu hususani wanaofanya kazi za kilimo katika bonde la Ziwa Eyasi kutunza miti iliyopandwa kwa lengo la kulinda mazingira .

Amesema hayo alipokuwa akizundua zoezi la upandaji Miti katika Wilaya hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella.

Mhe.Kolimba amesema wameamua kupanda miti takribani 1000 ili kuunga mkono juhudi za Rais wa Tanzania Mhe.Dkt.Samia za kulinda mazingira lakini pia kutekeleza maelekezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuwa kila Wilaya ihakikishe inapanda miti milioni moja na nusu ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi.

Aidha,Mhe.Kolimba amesema kuwa eneo la bonde la mto Baray limekuwa chanzo kikuu cha maji kwa ajili ya umwagiliaji mkubwa wa zao vitunguu kwa wakulima wa Kijiji cha Mbuga Nyekundu Wilayani Karatu.

“Nakuagiza Afisa Mazingira wa Halmshauri simamieni suala la utunzaji mazingira kwa kusimamia sheria za utunzaji mazingira ili kubaini Wale wote wanaoharibu mazingira kwa kukata miti hivyo.”

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Karatu Dkt. John Mahu amesema Halmashauri hiyo imetenga kiasi cha Milioni 54 kwa ajili zoezi la upandaji Miti katika maeneo mbalimbali ndani ya Wilaya ya Karatu.

Naye, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Karatu bwana Karia Rajabu amesema suala la upandaji miti ni endelevu na kuwa Halmashauri itahakikisha inatumia vizuri msimu wa mvua za masika kupanda miti kwa wingi na kuongeza kuwa Watumishi wote watapewa jukumu la kusimamia utunzaji miti.

Zoezi la upandaji Miti katika Halmashauri ya Karatu ni mwendelezo wa kuhakikisha inatimiza lengo la kupanda miti 1,500,000 kwa mwaka 2022/2023.

# NYUMBA YA WAGENI



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akiteta jambo na mwenyeji wake Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John V.K Mongella mara baada ya kuwasili katika uwanja cha ndege wa Kisongo Jijini Arusha.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe.John V.K Mongella akiteta jambo na Balozi wa Burundi Nchini Tanzania Mhe. Gervais Abayeho ambaye aliwasili Mkoani Arusha kwa ziara ya kikazi.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongella akiwa katika mazungumzo na Bi. Kate Somvongsiri Mkurugenzi Mkazi wa USAID Nchini Tanzania aliewasili Mkoani Arusha kwa ziara ya kikazi.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John V.K Mongella (wa nne kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Mabalozi kutoka Nchi za Afrika wenye uwakilishi Nchini Tanzania ambao wapo Mkoani Arusha kwa ziara ya kikazi



Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongella akiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mhe. Makongoro Nyerere alipotembelea ofisini kwake, kulia ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha Bw. Missaile Musa.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akiteta jambo na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa ambaye yupo Mkoani Arusha kwa ziara ya kikazi.